JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

# HOTUBA YA JAJI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA **MHE. GEORGE M. MASAJU, SIKU YA SHERIA NCHINI**

**TAREHE 2 FEBRUARI, 2026**
**DODOMA – TANZANIA**



**KAULI MBIU:**
***"Mchango wa Mahakama katika Ustawi na Maendeleo ya Taifa"***

# HOTUBA YA JAJI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# **MHE. GEORGE M. MASAJU, SIKU YA SHERIA NCHINI**

## TAREHE 2 FEBRUARI, 2026
## DODOMA – TANZANIA

**KAULI MBIU:**

“Mchango wa Mahakama katika Ustawi na Maendeleo ya Taifa”

Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Mhe. Augustine Mwarija, Jaji wa Mahakama ya Rufani na Amidi wa Mahakama ya Rufani,

Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani,
Mhe. Khamis Ramadhani Abdallah, Jaji Mkuu wa Zanzibar,
Mhe. Dkt. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi,
Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera, Waziri wa Katiba na Sheria,
Mhe. Jaji Madibo Sacko, Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu,
Mhe. Jaji Nestor Kayobera, Rais wa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki,

Mhe. Yohanne Bokobora Masara, Jaji Kiongozi wa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki,

Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu,

Wahe. Mawaziri Prof. Riziki Shemdoe na Balozi Mussa Ommar,

Mhe. Hamza Saidi Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
Wahe. Majaji Viongozi Wastaafu mliopo,
Wahe. Majaji Wastaafu mliopo,

Mhe. Baraka Leonard, Katibu wa Bunge,
Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania,

Mhe. Khai Mbaraouk, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Zanzibar,
Mhe. Eva Kiaki Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania,

Mhe. Valentina Katema, Mrajisi, Mahakama ya Zanzibar,

Bw. Silvester Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka,
Mhe. Dkt. Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma,
Wakili Boniface Anyisile Kajunjumele

Mwabukusi,Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika,
Viongozi Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama,
Wahe. Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa,
Wahe. Wasajili, Naibu Wasajili,
Wakurugenzi na Watendaji wa Mahakama,
Wahe. Mahakimu na Mawakili,
Viongozi wa Vyama vya Siasa,
Viongozi wa Dini,

Ndugu wanahabari,
Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana,

**Mheshimiwa Rais**, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na fadhili, kwa kutujalia afya njema na kutukutanisha kwa mara nyingine tena katika siku hii muhimu kwa Mahakama ya Tanzania, baada ya mwaka mmoja wa tukio kama hili lililofanyika tarehe 3 Februari, 2025.

Kwa niaba ya Mahakama ya Tanzania, natoa shukrani za dhati kwako kwa kukubali mwaliko wetu wa kuwa Mgeni Rasmi katika Siku ya Sheria Nchini bila kujali ratiba yako muhimu lakini bila kujali pia kuwa ulikuwa nasi wiki tatu zilizopita katika Mkutano Mkuu wa chama cha Mahakimu na Majaji (TMJA). Hii inathibitisha kuwa unaiheshimu, unaithamini na kuijali Mahakama ya Tanzania. Na hapa Mheshimiwa Rais naomba nikudokeze tu kwamba, neno lako la matumaini ulilolitoa siku hiyo ya tarehe 13 Januari, 2026 pamoja na kuridhia mabadiliko mbalimbali ya sheria tuliyopendekeza ambayo ni kwa ajili ya kurahisisha na kuharakisha upatikanaji wa haki mapema ipasavyo vimeongeza ari na hamasa ya kazi kwa Watumishi wa Mahakama.

**Mheshimiwa Rais**, ninakupongeza kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 8(1)(a) ya Katiba kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Uchaguzi Mkuu, 2025. Mwenyezi Mungu aendelee kukubariki katika maisha, utumishi na shughuli za umma katika utekelezaji wa majukumu yako ya kikatiba, kisheria na kisera.

**Mheshimiwa Rais**, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninakushukuru Mheshimiwa Spika kwa ushirikiano hata kiasi cha kuweza kutenga muda wako kuungana nasi licha ya shughuli zako nyingi katika kipindi hiki cha Mkutano wa Bunge unaoendelea hapa Jijini Dodoma. Ninakutakia kila la kheri katika maisha, utumishi na shughuli za umma.

**Mheshimiwa Rais**, napenda kuwakaribisha na kuwashukuru Viongozi na Wageni wote waalikwa kwa kukubali mwaliko na kutenga muda wao kushiriki nasi kwenye maadhimisho haya ya Siku ya Sheria Nchini Mwaka 2026. Kwa kuwa tunakutana kwa mara ya kwanza katika Mwaka wa Kazi wa Mahakama, ninawatakieni kila la kheri watumishi wote wa Mahakama ya Tanzania katika Mwaka huu wa Kazi 2026. Tunawatakieni kila la kheri, viongozi na wananchi wote katika maisha, utumishi na shughuli za kazi.

**Mheshimiwa Rais**, kauli mbiu inayotuongoza katika maadhimisho ya mwaka huu 2026 ni **"MCHANGO WA MAHAKAMA KATIKA USTAWI NA MAENDELEO YA TAIFA"**. Kauli mbiu hii inakusudiwa kutoa fursa kwa Mahakama na wadau wake kutafakari, kujadili na kudumisha mchango wa Mahakama katika ustawi na maendeleo ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Rais**, Ibara ya 8(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Katiba), inaelekeza kwamba lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi. Kwa mujibu wa Ibara ya 4 ya Katiba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inajumuisha Mahakama. Kwa hiyo, Mahakama inao wajibu wa kikatiba katika kuchangia ustawi na maendeleo ya Taifa la Jamhuri ya Muungano kama linavyotajwa katika Ibra ya 1 na 2(1) ya Katiba.

**Mheshimiwa Rais**, mambo makuu yanayounda ustawi na maendeleo ya Taifa yametajwa katika Ibara ya 6-11 ya Katiba. Mambo hayo ndiyo yanayounda masharti mengineyo yote katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Na kwa sababu hiyo, mambo hayo yamesisitizwa na kulindwa katika Ibara ya 19(3) na 30(2) ya Katiba. Hata Mahakama huru inapokuwa

inatekeleza jukumu lake la kutoa haki inawajibika kuzingatia, kutia maanani na kutekeleza masharti hayo ipasavyo kama ambavyo Ibara ya 7(1) na 107B ya Katiba zinavyoelekeza. Kimsingi mambo hayo ndiyo yanayounda usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii na umoja wa kitaifa na ndiyo maslahi ya haki, maslahi ya umma na maslahi ya taifa.

**Mheshimiwa Rais**, Mahakama inapokuwa inatekeleza ipasavyo jukumu lake la utoaji haki kwa mujibu wa Ibara 4, 107A na 107B ya Katiba, inachangia ustawi na maendeleo ya Taifa kwa sababu uwepo wa haki katika maamuzi ya Mahakama inachangia amani na udugu wa wananchi na hivyo kuwawezesha wananchi kuendelea na shughuli zao za kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa ufanisi ipasavyo na hivyo kusonga mbele katika ustawi na maendeleo ya Taifa. Kwa hiyo, watumishi wa Mahakama hususan waamuzi

(Majaji na Mahakimu) tunapoviishi viapo vyetu vya ofisi na uadilifu yaani kuzingatia Katiba, sheria na maadili ya utumishi wetu, tunawezesha Mahakama kuchangia ipasavyo katika ustawi na maendeleo ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Rais,** Haki maana yake ni uamuzi unaofanywa na mahakama kwa kuzingatia masharti ya Katiba na sheria za nchi kwa mujibu wa ushahidi unaowasilishwa Mahakamani.

**Mheshimiwa Rais**, Mahakama inachangia ustawi na maendeleo ya Taifa inapokuwa inadumisha Utawala wa Sheria kwa mujibu wa Ibara 26 ya Katiba kwa kuwaadhibu na kuwawajibisha ipasavyo wanaokiuka masharti ya Katiba na Sheria za Taifa letu kwa mujibu wa ibara 107A na ibara 107B ya Katiba.

**Mheshimiwa Rais,** kutokana na mchango na umuhimu wa Mahakama katika ustawi na maendeleo ya Taifa, ndiyo maana heshima, mamlaka na uhuru wa Mahakama vimehifadhiwa na kulindwa katika Ibara ya 30(2)(d) ya Katiba. Kifungu cha 114 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu (The Penal Code) kinawawajibisha watu wanaodharau Mahakama, mamlaka na uhuru wake.

**Mheshimiwa Rais,** tunakupongeza kwa kuendelea kuiheshimu Mahakama, mamlaka na uhuru wake kwa kauli na vitendo hata kudhamiria kwa vitendo kuiwezesha Mahakama ya Tanzania ifikie kuwa yenye hadhi duniani. Tunakushukuru sana kwa hatua unazochukua kwa ajili hiyo.

**Mheshimiwa Rais**, ili Mahakama iweze kutekeleza jukumu lake la kikatiba na hivyo kuchangia katika ustawi wa wananchi,

huduma zetu za Mahakama lazima ziwepo nchini kote, kuanzia angalau ngazi ya Kata hadi ngazi ya Taifa. Tunaipongeza Serikali kwa hatua za ujenzi wa mahakama za ngazi zote nchini. Hatua hii inachochea, kuongeza na kukuza mchango wa Mahakama katika ustawi na maendeleo ya Taifa kwa kuwa wananchi wenye migogoro wanaifikia Mahakama kwa ukaribu na wanaokiuka Katiba na sheria kuwajibishwa mapema kwa mujibu wa ibara ya 26 ya Katiba.

**Mheshimiwa Rais, Majedwali A,B,C,D** na **E** yameonyesha Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama kuanzia mwaka 2020 hadi sasa. Na hivi karibuni tarehe 13 Januari, 2026 ulielekeza kwamba Serikali itaanza kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama za Mwanzo katika kila kata ambako hakuna huduma za Mahakama hiyo; na kwamba mradi huo wa ujenzi wa Mahakama za Mwanzo

utatekelezwa kwa namna ambayo miradi ya ujenzi wa Shule za msingi na Sekondari, Zahanati na Vituo vya Afya na Hospitali ilivyotekelezwa kwa mafaniko makubwa na TAMISEMI. Tunakupongeza kwa mafanikio hayo makubwa katika sekta ya elimu, afya na maji. Kwa hiyo, TAMISEMI ndio wapo katika nafasi nzuri zaidi ya utekelezaji wa mradi huu kuliko Mahakama. Mahakama itashirikiana na TAMISEMI kwa kuwapatia Ramani ya Majengo ya Mahakama na Nyumba za Mahakimu katika Mahakama hizo za Mwanzo.

**Mheshimiwa Rais**, kimsingi TAMISEMI ndio wanaowajibika kutekeleza Mradi huu kwa sababu kwa mujibu wa Ibara ya 146(2)(b) ya Katiba, Serikali za Mitaa wanalo jukumu la kuhakikisha utekelezaji wa sheria na ulinzi wa wananchi katika maeneo yao, yaani kuimarisha Utawala wa Sheria katika Serikali za Mitaa. Kwa sababu hiyo, huduma

za Mahakama zinahitajika katika maeneo hayo kwa mujibu wa Ibara 26(2) ya Katiba.

**Mheshimiwa Rais**, **Jedwali "G"** linaonyesha majengo yanayokarabatiwa ambayo yalikuwa Mahakama Kuu. Majengo hayo yanakusudiwa kuwa Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki kwa mashauri ya Mirathi, Ndoa na Talaka kama ilivyo kwenye Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki, Temeke. Uzoefu wa kituo Jumuishi cha Utoaji Haki, **Temeke** ambao umeleta ufanisi mkubwa katika kushughulikia mashauri ya aina hiyo umetusukuma kuanzisha vituo kama hicho kwa baadhi ya Mikoa/Kanda za Mahakama.

**Mheshimiwa Rais,** Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki ambavyo viko katika hatua za kukamilika ili vianze kutoa huduma mwezi Machi, 2026 ni vituo saba kama **Jedwali "A"** linavyoonyesha. Jedwali hilo pia linataja

vituo vingine Jumuishi vya Utoaji Haki ambavyo tayari vimekamilika na vinatoa huduma. Vituo Jumuishi vya Haki ambavyo viko katika hatua ya kukamilika ili vianze kutoa huduma mwezi Machi 2026 ni Njombe, Katavi, Singida, Pemba, Songwe, Lindi na Songea.

**Mheshimiwa Rais,** katika kuimarisha usimamizi wa utoaji haki, kuanzia tarehe 15 Juni, 2025 hadi tarehe 15 Desemba, 2025 tumetunga jumla ya Kanuni (*Rules*) kumi na moja (11). Kanuni hizo ni pamoja na: Kanuni za Usimamizi wa Mirathi (*The Primary Courts (Administration of Estates) (Amendments) Rules, 2025* GN. No. 428 of 2025, *The Probate (Amendment) Rules, 2025* GN. No. 429 of 2025), *Instrument of Determination of Judges to Serve in the Corruption and Economic Crimes Division of the High Court of the United Republic*, Taarifa ya Kawaida Na. 9330 ya 2025, *Kanuni za Ulinzi wa Mashahidi, 2025*

TS Na. 430 la 2025, *The Judicature and Application of Laws (Constitutional Petitions) (Practice and Procedure) Rules, 2025* GN. No. 540 of 2025, *The Judicature and Application of Laws (Panel Constitution) Rules, 2025* GN. No. 541 of 2025, *The Civil Procedure Code (Amendment of the First Schedule), Rules 2025* GN. No. 569 of 2025, *The Judicature and Application of Laws (Defence Entitlement to Prosecution Evidence) Rules 2025* GN. No. 597 of 2025, na *The Judicature and Application of Laws (Electronic Filing) (Amendment) Rules, 2025* GN. No. 609 of 2025. Taarifa zaidi kuhusu Kanuni hizi pamoja na nyinginezo, sababu na faida zake ni kama ilivyoelezwa kwenye **Jedwali "F"** katika hotuba hii.

**Mheshimiwa Rais**, sambamba na utungaji na urekebishaji wa Kanuni, Mahakama ya Tanzania imeimarisha haki ya watuhumiwa wenye stahili ya kisheria kupata dhamana, kupata dhamana ipasavyo mahakamani

kuanzia mahakama za mwanzo ambako kwa sasa dhamana inapatikana kwa watuhumiwa/washtakiwa wote katika Mahakama za Mwanzo. Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo zinawajibika kuhakikisha kuwa dhamana inatolewa kwa washtakiwa kwa mashauri yote ya jinai yenye dhamana isipokuwa kama kuna sababu ya msingi. Mtu anapoomba dhamana uamuzi wa kumpa au kumkatalia dhamana utolewe siku hiyo ya kuwasilisha ombi lake Mahakamani. Hii inasaidia kupunguza mianya ya rushwa lakini pia inawezesha haki ya dhamana kupatikana mapema ipasavyo. Kwa makosa ambayo kisheria yanadhaminika, Waheshimiwa Mahakimu wanawajibika kuwajulisha watuhumiwa haki ya dhamana mara tu watuhumiwa wanapofikishwa mbele yao. Hatua hii inawawezesha wananchi wanaotuhumiwa kwa makosa ya jinai kuendelea na shughuli zao za kiuchumi na kijamii na kuhudhuria

Mahakamani wakitokea nyumbani hadi mashtaka dhidi yao yanapokuwa yametolewa hukumu/maamuzi mahakamani ipasavyo kwa mujibu wa Ibara 13(6)(b) ya Katiba.

**Mheshimiwa Rais**, hatua kuhusiana na dhamana kwa washtakiwa/watuhumiwa zimepunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani na kuleta unafuu katika gharama za uendeshaji wa magereza.

**Mheshimiwa Rais,** tunaendeleza na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za Mahakama ili kuimarishaufanisi. Hivisasatunajengamfumo unaotumia Akili Unde (*Artificial Intelligence*) kwa ajili ya kuchukua/kurekodi mwenendo wa kumbukumbu za mashauri na Hukumu Mahakamani. Katika mfumo huo, Jaji, Hakimu, Wakili, Shahidi nk wanapotamka au kuzungumza Mahakamani, mfumo huo

unatafsiri lugha iliyotumika na kuiandika kwa lugha inayokuwa imechaguliwa kuandikwa (*Translation & Transcription*) wakati huo huo. Mfumo huo utakapokuwa umeanza kutumika, utaimarisha sana ufanisi wa utendaji wa Mahakama kwani kuchukua kumbukumbu za mwenendo wa mashauri Mahakamani kwa kuandika kwa mkono au kompyuta kunachelewesha na kuchosha na wakati fulani hata kupotosha. Tutaendeleza na kuimarisha utaratibu wa kusikiliza mashauri kwa njia ya mtandao (*online litigation*) na hivyo kuleta unafuu katika gharama na kupunguza usumbufu kwa wadaawa wa mashauri Mahakamani.

**Mheshimiwa Rais,** Dira ya Mahakama ni "**Haki sawa kwa wote mapema ipasavyo** (*Timely and accessible justice for all*). Msingi wa Dira hii ni Ibara ya 107A(1)(2)(a)(b) na ibara 107B ya Katiba. Mojawapo ya nguzo za Dira ya Mahakama ni huduma zinazomlenga

mwananchi (*Citizen Centric Service*). Ndiyo maana Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa Mahakama za ngazi zote nchini, ikiwemo ujenzi wa Mahakama za Mwanzo kila kata ili kusogeza huduma za Mahakama kwa wananchi kusudi huduma za Mahakama ziweze kufikika kwa urahisi ikizingatiwa pia kwamba asilimia 70% ya mashauri yote Mahakamani ni yale ya Mahakama za Mwanzo. Serikali imejenga vituo Jumuishi vya Utoaji Haki (*Intergrated Justice Centres – IJC*) ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za Mahakama kwa ukaribu zaidi. Katika vituo hivyo kunakuwa na Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakimu Mkazi/Mkoa, Mahakama Kuu na Ofisi (*Chambers*) za Waheshimiwa Majaji wa Rufani. Hata Jengo la Makao Makuu ya Mahakama ni Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki, kwani hapo kuna Mahakama Kuu, Mahakama ya Rufani na nafasi ya Mahakama ya Juu zaidi (*Supreme Court*) itakapokuwa imeanzishwa. Na kwa muda

mrefu sasa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani zimekuwa na utaratibu mzuri tu wa uendeshaji vikao vyake Wilayani na Mikoani mtawalia katika Kanda ili kusogeza zaidi huduma zake kwa wananchi.

**Mheshimiwa Rais**, kwa sababu hizo na kwa kuzingatia mchango muhimu wa Mahakama katika ustawi na maendeleo ya Taifa, tunafanya ugatuzi wa Mahakama ya Rufani ili sasa Mahakama hii ya juu kabisa nchini iweze kuwepo katika baadhi ya Kanda za Mahakama nchini ambazo tayari zina Masjala Ndogo.

**Mheshimiwa Rais**, pamoja na mengine, hatua hii ya ugatuzi itaimarisha umuhimu wa Mahakama ya Rufani kwa wananchi. Kwa sababu hiyo Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani, Naibu Wasajili na watumishi wote wa Mahakama ya Rufani watakao kuwa katika Ofisi za Kanda wataendelea kupata haki na stahili zao

za utumishi ipasavyo kama ilivyo kwa watumishi watakaokuwa Makao Mkuu, Dodoma. Lengo la ugatuzi huu ni kusogeza tu huduma za Mahakama karibu na wananchi, ili kuwezesha haki kupatikana mapema ipasavyo. Katika ugatuzi huu sasa baadhi ya Waheshimiwa Majaji watafanya kazi wakiwa katika Masjala za Kanda kama Dar es Salaam, ambayo itahudumia pia Zanzibar kabla ya kuanzishwa kwa masjala nyingine ya kudumu Zanzibar. Kanda nyingine ni Arusha, Mwanza, Mbeya na Tabora.

**Mheshimiwa Rais,** kama tulivyokwisha ona Mahakama inao mchango mkubwa katika ustawi na maendeleo ya Taifa kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kwa upande wa uchumi, mwaka 2025 Mahakama katika baadhi ya mashauri ya kiuchumi yaliyosikilizwa kama yanavyotajwa katika **Jedwali "H"** kwa mujibu wa Hati za Madai na Hati za Rufaa, yalifikia thamani ya TShs 50,441,708,274,962/=.

Miongoni mwa fedha hizo TShs 13 trilioni ikiwa ni kwa mashauri yaliyosikilizwa na kumalizika mwezi Oktoba hadi Desemba, 2025. Bila shaka kwa fedha zilizoingia katika matumizi na biashara mara baada ya mashauri hayo kuhitimishwa Mahakamani zimechangia kukuza biashara na uwekezaji (Uchumi) na hivyo ustawi na maendeleo ya Taifa.

**Mheshimiwa Rais**, tunachukua hatua ipasavyo kuifanya Mahakama kuendelea kuwa mahali pa kupata haki mapema ipasavyo na siyo mahali pa kuegesha mashauri baina ya Wadaawa kama ambavyo wadaawa wasiokuwa waaminifu wamekuwa wakikwepa kuwajibika kimikataba na kisheria katika mashauri ya Madai kwa aina zake zote. Ili tufanikiwe katika azima hii wadau wote muhimu wa Mahakama hususan wadaawa wenyewe, mawakili na mashahidi wao wanawajibika kutoa ushirikiano

ipasavyo kwa Mahakama kwa mujibu wa Katiba, sheria na maadili ya mawakili wote. Kimsingi, Mawakili ni Maafisa wa Mahakama (*Court Officers*), siyo wanaharakati wa upande wowote katika mashauri Mahakamani. Tunachukua hatua ipasavyo kuimarisha nidhamu, mwenendo na uwajibikaji wa mawakili Mahakamani, ikiwa ni pamoja na kuiboresha Sheria ya Mawakili ili kutunza heshima, mamlaka na uhuru wa Mahakama kwa mujibu wa Ibara 30(2)(d) ya Katiba. Madalali (*Court Brokers and Auctioneers*) nao wanawajibika kuzingatia Katiba, sheria, maadili yao na Hukumu/Amri za mahakama. Vinginevyo, madalali wasiokuwa waadilifu wanakuwa wanashiriki dhuluma na uhalifu. Wanapaswa kuwajibishwa hata kwa kushtakiwa Mahakamani ipasavyo.

**Mheshimiwa Rais,** Msingi Mkuu wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ni Utawala (Governance), Amani (*Peace*), Usalama

(*Security*) na Utulivu (*Stability*). Maeneo ya Kipaumbele (*Attributes*) katika Msingi Mkuu wa Dira ni Utawala Bora na Haki (*Good Governance and Justice*), Serikali za Mitaa Imara na zenye ufanisi (*Strong and Effective Local Governance*), Utumishi wa Umma Unaowajibika (*Responsible and Accountable Public Service*) na Amani, Usalama na Utulivu (*Peace, Security and Stability*). Kwa Msingi Mkuu wa Dira na vipaumbele vyake ambavyo kimsingi ni masuala ya Utawala wa Sheria na Haki na ambapo Mahakama ni mhusika mkuu kwa mujibu wa Ibara ya 4, 26, 107A na 107B ya Katiba, ni dhahiri kwamba Mahakama itaendelea kuwa na mchango muhimu katika ustawi na maendeleo ya Taifa katika muktadha wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 pia.

**Mheshimiwa Rais,** ili Mahakama iweze kutekeleza jukumu na wajibu wake katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo

2050 na kuchangia ipasavyo katika Ustawi na maendeleo ya Taifa kwa mujibu wa majukumu yake kikatiba; sisi watumishi wote wa Mahakama ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mbali na kuzingatia Katiba, Sheria, Viapo, Maadili ya Utumishi wa Mahakama/Umma, Mila na Desturi za Mahakama; tunalazimika na tutalazimika kuzingatia na kuishi vitendea kazi vya kiakili, kiroho na kimwili yaani tabia ambayo ni kama *software* katika utendaji wetu.

**Mheshimiwa Rais,** vitendea kazi hivyo vya kiakili/kitabia ni: **kuwiwa kuona haki inatendeka na kuitenda ipasavyo** (*sensitivity to justice*), **uadilifu** (*integrity*), **uwezo wa kumudu utekelezaji wa majukumu ipasavyo** (*competency*), **uchukuaji hatua mapema/ kujituma** (*pro-activity*), **ubunifu** (*creativity*), **uzalendo** (*national patriotism*), **uhalisia / ukweli usioegemea upande wowote** (*objectivity*) na **uwajibikaji** (*accountability*). Hiki kitendea kazi cha mwisho (**uwajibikaji**)

kinabeba na kufungamanisha vitendea kazi vingine vyote, kwa maana kwamba, kila mtumishi akiwajibika ipasavyo atakuwa pia anatekeleza na hivyo vitendea kazi vingine saba na hivyo kuweza kutimiza nidhamu ya kazi. Kitendea kazi hiki pia kimeelezwa vizuri kwenye ibara ya 25 ya Katiba**.** Utumishi wa Umma Unaowajibika ni kipaumbele cha tatu katika Msingi Mkuu wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Mbali ya Katiba, Sheria na Maadili ya utumishi wa Mahakama vitendea kazi hivi pia vimetajwa katika kifungu cha 6 cha Sheria ya maadili ya Viongozi wa Umma.

**Mheshimiwa Rais,** baada ya kusema hayo sasa naomba nikukaribishe uweze kuongea na hadhara hii pamoja na wananchi kwa ujumla na kisha utuzindulie rasmi mwaka wa kazi wa Kimahakama kwa Mwaka 2026. Mheshimiwa Rais karibu sana.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**

## JEDWALI "A": VITUO JUMUISHI VYA UTOAJI HAKI (IJCs)

| Na. | Jina la Mradi | Wilaya | Mkoa | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 1 | IJC- ARUSHA | Arusha Mjini | Arusha | Kazi zimekamilika na jengo linatumika |
| 2 | IJC- DODOMA | Dodoma Mjini | Dodoma | |
| 3 | IJC- MOROGORO | Morogoro Mjini | Morogoro | |
| 4 | IJC- MWANZA | Ilemela | Mwanza | |
| 5 | IJC- KINONDONI | Kinondoni | Dar es Salaam | |
| 6 | IJC- TEMEKE | Temeke | Dar es Salaam | |
| 7 | IJC- SIMIYU | Bariadi | Simiyu | |
| 8 | IJC- GEITA | Geita | Geita | |
| 9 | IJC- NJOMBE | Njombe Mjini | Njombe | Majengo yanategemewa kuwa tayari kwa matumizi Machi 2026 |
| 10 | IJC- KATAVI | Mpanda | Katavi | |
| 11 | IJC- SINGIDA | Singida | Singida | |
| 12 | IJC- PEMBA | Chakechake | Kusini Pemba | |
| 13 | IJC- SONGWE | Songwe | Songwe | |
| 14 | IJC- LINDI | Lindi | Lindi | |
| 15 | IJC- SONGEA | Songea | Ruvuma | |

## JEDWALI "B": MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI

| Jina la Mradi | Wilaya | Mkoa | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| Ofisi za Hakimu Mkazi - Songwe | Songwe | Songwe | Kazi zimekamilika na majengo yanatumika |
| Ofisi za Hakimu Mkazi - Katavi | Katavi | Katavi | |
| Ofisi za Hakimu Mkazi - Njombe | Njombe Mjini | Njombe | |
| Ofisi za Hakimu Mkazi - Lindi | Lindi Mjini | Lindi | |

## JEDWALI "C": MAHAKAMA ZA WILAYA

| Na. | Jina la Mahakama ya Wilaya | Wilaya | Mkoa | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ngara | Ngara | Kagera | Kazi zimekamilika na majengo yanatumika |
| 2 | Namtumbo | Namtumbo | Ruvuma | |
| 3 | Same | Same | Kilimanjaro | |
| 4 | Mwanga | Mwanga | Kilimanjaro | |
| 5 | Nanyumbu | Nanyumbu | Mtwara | |
| 6 | Tandahimba | Tandahimba | Mtwara | |
| 7 | Chemba | Chemba | Dodoma | |
| 8 | Bahi | Bahi | Dodoma | |
| 9 | Kaliua | Kaliua | Tabora | |
| 10 | Uvinza | Uvinza | Kigoma | |
| 11 | Buhigwe | Buhigwe | Kigoma | |
| 12 | Kakonko | Kokonko | Kigoma | |
| 13 | Butiama | Butiama | Mara | |
| 14 | Rorya | Rorya | Mara | |
| 15 | Itilima | Itilima | Simiyu | |
| 16 | Busega | Busega | Simiyu | |
| 17 | Songwe | Songwe | Songwe | |
| 18 | Tanganyika | Tanganyika | Katavi | |
| 19 | Mbogwe | Mbogwe | Geita | |
| 20 | Nyang'wale | Nyang'wale | Geita | |
| 21 | Kyerwa | Kyerwa | Kagera | |
| 22 | Misenyi | Misenyi | Kagera | |
| 23 | Gairo | Gairo | Morogoro | |
| 24 | Mvomero | Mvomero | Morogoro | |
| 25 | Kilombero | Kilombero | Morogoro | |
| 26 | Mkinga | Mkinga | Tanga | |
| 27 | Kwimba | Kwimba | Mwanza | |
| 28 | Liwale | Liwale | Lindi | |
| 28 | Manyoni | Manyoni | Singida | |
| 30 | Korogwe | Korogwe | Singida | |
| 31 | Ulanga | Kibaigwa | Dodoma | |

| Na | Jina la Mahakama ya Wilaya | Wilaya | Mkoa | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 32 | Kibiti | Kibiti | Pwani | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Juni 2026 |
| 33 | Hanang | Hanang | Manyara | |
| 34 | Simanjiro | Simanjiro | Manyara | |
| 35 | Nanchingwea | Nachingwea | Lindi | |
| 36 | Tunduru | Tunduru | Ruvuma | |
| 37 | Mbulu | Mbulu | Manyara | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Oktoba 2026 |
| 38 | Chamwino | Chamwino | Dodoma | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Juni 2026 |
| 39 | Mkalama | Mkalama | Singida | |
| 40 | Uyui | Uyui | Tabora | |
| 41 | Kilosa | Kilosa | Morogoro | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Februari 2026 |
| 42 | Nyasa | Nyasa | Ruvuma | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Juni 2026 |
| 43 | Masasi | Masasi | Mtwara | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Mei 2026 |
| 44 | Kishapu | Kishapu | Shinyanga | |
| 45 | Tarime | Tarime | Mara | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Aprili 2026 |
| 46 | Kalambo | Kalambo | Rukwa | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Mei 2026 |
| 47 | Ukerewe | Ukerewe | Mwanza | |
| 48 | Biharamulo | Biharamulo | Kagera | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Agusti 2026 |
| 49 | Lushoto | Lushoto | Tanga | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi August 2026 |

| Na. | Jina la Mahakama ya Wilaya | Wilaya | Mkoa | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 50 | Handeni | Handeni | Tanga | Miradi hii iko kwenye hatua ya manunuzi |
| 51 | Igunga | Igunga | Tabora | |
| 52 | Mlele | Mlele | Katavi | |
| 53 | Rufiji | Rufiji | Pwani | |
| 54 | Kiteto | Kiteto | Manyara | |
| 55 | Ubungo | Ubungo | Dar es Salaam | Kazi zimekamilika na jengo linatumika. |

## JEDWALI "D": MAHAKAMA ZA MWANZO

| Na. | Jina la Mahakama ya Mwanzo | Wilaya | Mkoa | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Hydom | Mbulu | Manyara | Kazi zimekamilika na majengo yanatumika |
| 2. | Kimbe | Kilindi | Tanga | |
| 3. | Nyakibimbili | Bukoba Vijijini | Kagera | |
| 4. | Matiri | Songea | Ruvuma | |
| 5. | Kabanga | Ngara | Kagera | |
| 6. | Chanika | Ilala | Dar es Salaam | |
| 7. | Kinesi | Rorya | Mara | |
| 8. | Madale | Kinondoni | Dar es Salaam | |
| 9. | Luilo | Ludewa | Njombe | |
| 10. | Usevya | Mlele | Katavi | |
| 11. | Newala | Newala | Mtwara | |
| 12. | Mahenge | Kilolo | Iringa | |
| 13. | Izigo | Muleba | Kagera | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Machi 2026 |
| 14. | Nyakakika | Karagwe | Kagera | |
| 15. | Kigoma Kaskazini | Kigoma Ujiji | Kigoma | |
| 16. | Heru Juu | Kasulu | Kigoma | |
| 17. | Manyovu | Buhigwe | Kigoma | |
| 18. | Mipingo | Lindi Mjini | Lindi | Kazi zimekamilika na majengo yanatumika |
| 19. | Mtandi | Masasi | Mtwara | |
| 20. | Ndomoni | Nachingwea | Lindi | |
| 21. | Chikundi | Masasi | Mtwara | |

| Na. | Jina la Mahakama ya Mwanzo | Wilaya | Mkoa | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 22. | Msata | Chalinze | Pwani | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Machi 2026 |
| 23. | Bungu | Kibiti | Pwani | |
| 24. | Somangila | Kigamboni | Pwani | |
| 25. | Kimanzichana | Mkuranga | Pwani | |
| 26. | Mbagala | Temeke | Dar es Salaam | |
| 27. | Inonelwa | Misungwi | Mwanza | |
| 28. | Kabila | Magu | Mwanza | |
| 29. | Nyatukala | Sengerema | Mwanza | |
| 30. | Muganza | Chato | Geita | |
| 31. | Tarakea | Rombo | Kilimanjaro | |
| 32. | Terrat | Arusha | Arusha | |
| 33. | Gonja | Same | Kilimanjaro | |
| 34. | Sanja Juu | Siha | Kilamanjro | |
| 35. | Terat | Simanjiro | Manyara | |
| | | | | Kazi zimekamilika na majengo yanatumika |
| 36. | Maji ya Chai | Meru | Arusha | |
| 37. | Makuyuni | Monduli | Arusha | |
| 38. | Minjingu | Babati | Manyara | |
| 39. | Mugumu | Serengeti | Mara | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Machi 2026 |
| 40. | Ngulyati | Bariadi Mjini | Simiyu | |
| 41. | Nyalikungu | Maswa | Simiyu | |
| 42. | Lugangabilili | Itilima | Simiyu | |
| 43. | Majengo | Shinyanga Mjini | Shinyanga | Kazi zimekamilika na majengo yanatumika |
| 44. 45 | Malunga | Kahama | Shinyanga | |
| 45. 46 | Nganzo | Bukombe | Geita | |
| 46. 47 | Unyamikubi | Singida Urban | Singida | |
| 47. 48 | Minyunge | Ikungi | Singida | |
| 48. 49 | Kwamtoro | Chemba | Dodoma | |
| 49. 50 | Bwakila Chini | Morogoro Vijijini | Morogoro | |
| 50. | Minepa | Malinyi | Morogoro | |

| Na. | Jina la Mahakama ya Mwanzo | Wilaya | Mkoa | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 51. | Kasanga | Kalambo | Rukwa | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Machi 2026 |
| 52. | Namanyere | Nkasi | Rukwa | |
| 53. | Nambogo | Sumbawanga | Rukwa | |
| 54. | Ugala | Mlele | Katavi | |
| 55. | Sibwesa | Tanganyika | Katavi | |
| 56. | Mamba | Mpimbwe | katavi | |
| 57. | Rujewa | Mbalali | Mbeya | Kazi zimekamilika na majengo yanatumika |
| 58. | Lupatingatinga | Chunya | Mbeya | |
| 59. | Ndobo | Kyela | Mbeya | |
| 60. | Kanga | Songwe | Songwe | |
| 61. | Msangano | Mbozi | Songwe | |
| 62. | Chikongola | Mikindani | Mtwara | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Machi 2026 |
| 63. | Kitangari | Newala | Mtwara | |
| 64. | Nalasi | Tunduru | Ruvuma | |
| 65. | Likuyusekamaganga | Namtumbo | Ruvuma | |
| 66. | Lilondo | Madaba | Ruvuma | |
| 67. | Manda | Ludewa | Njombe | Kazi zimekamilika na majengo yanatumika |
| 68. | Lupembe | Njombe Vijijini | Njombe | |
| 69. | Izazi | Iringa Vijijini | Iringa | |
| 70. | Mafinga | Mafinga Urban | Iringa | |
| 71. | Ngoheranga | Malinyi | Morogoro | |
| 72. | Ketumbeine | Longido | Arusha | |
| 73. | Ilangala | Ukerewe | Mwanza | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Mei 2026 |
| 74. | Haubi | Kondoa | Dodoma | |
| 75. | Magubike | Kilosa | Morogoro | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Julai 2026 |
| 76. | Mbalizi | Mbeya Vijijini | Mbeya | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Juni 2026 |

| Na. | Jina la Mahakama ya Mwanzo | Wilaya | Mkoa | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 77. | Rungwa | Manyoni | Singida | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Mei 2026 |
| 78. | Mkuyuni | Nyamagana | Mwanza | |
| 79. | Machame | Hai | Kilimanjaro | |
| 80. | Nanjilinji | Kilwa | Lindi | |
| 81. | Kipili | Sikonge | Tabora | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Aprili 2026 |
| 82. | Kinusi | Mpwapwa | Dodoma | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Mei 2026 |
| 83. | Mkomazi | Same | Kilimanjaro | Mradi uko kwenye hatua za manunuzi. |
| 84. | Kibaigwa | Kongwa | Dodoma | Kazi imekamilika jengo linatumika |

## JEDWALI "E": MIRADI YA MATENGENEZO/UKARABATI WA MAJENGO YA MAHAKAMA

| Na. | Jina la Mradi | Wilaya | Mkoa | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mahakama Kuu - Tabora | Tabora | Tabora | Kazi zimekamilika na jengo linatumika |
| 2. | Mahakama Kuu - Moshi | Moshi | Kilimanjaro | |
| 3. | Mahakam aya Wilaya ya Maswa | Maswa | Simiyu | |
| 4. | Jengo la Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki – Musoma | Musoma | Mara | |
| 5. | Mahakama Kuu – Mwanza | Nyamagana | Mwanza | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Agusti 2026 |
| 6. | Mahakama Kuu - Iringa | Iringa | Iringa | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Julai 2026 |
| 7. | Mahakama Kuu - Dodoma | Dodoma Mjini | Dodoma | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Agusti 2026 |
| 8. | Mahakama ya Uhujumu Uchumi - Dar es Salaam | Ilala | Dar es Salaam | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Machi 2026 |
| 9. | Mahakama ya Hakimu Mkazi – Kisutu Renovation | Ilala | Dar es Salaam | Jengo linategemea kuwa tayari kwa matumizi Juni 2026 |

**JEDWALI "F": KANUNI ZILIZOTUNGWA NA KUREKEBISHWA 2025 NA FAIDA ZAKE**

| Na. | JINA LA KANUNI | Na. ya Tangazo la Serikali | TAREHE YA KUINGIA KWENYE MATUMIZI | MANUFAA YAKE KWA UMMA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | The Primary Courts (Administration of Estates) (Amendments) (Amendments) Rules, 2025 | GN No. 428 of 2025 | 11 Julai, 2025 | Kupunguza urasimu katika masuala ya mirathi.<br><br>Kuleta uwazi na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za mirathi<br><br>Kuweka udhibiti dhidi ya Wasisimamizi wa Mirathi wenye dhamira ya kutumia vibaya fedha au mali za marehemu.<br><br>Faida nyingine ni Mabenki ya biashara kupata wateja wanaotokana na utekelezaji wa kanuni inayotaka msimamizi wa mirathi kufungua akaunti maalumu za mirathi. |

MAHAKAMA YA TANZANIA
JUDICIARY OF TANZANIA

| Na. | JINA LA KANUNI | Na. ya Tangazo la Serikali | TAREHE YA KUINGIA KWENYE MATUMIZI | MANUFAA YAKE KWA UMMA |
|---|---|---|---|---|
| 2. | The Probate (Amendment) Rules, 2025 | GN No. 429 of 2025 | 11 Julai, 2025 | Kupunguza urasimu katika masuala ya mirathi.<br><br>Kuleta uwazi na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za mirathi<br><br>Kuweka udhibiti dhidi ya Wasisimamizi wa Mirathi wenye dhamira ya kutumia vibaya fedha au mali za marehemu.<br><br>Faida nyingine ni Mabenki ya biashara kupata wateja wanaotokana na utekelezaji wa kanuni inayotaka msimamizi wa mirathi kufungua akaunti maalumu za mirathi. |
| 3. | Instrument of Determination of Judges to Serve in the Corruption and Economic Crimes Division of the High Court of the United Republic | Taarifa ya Kawaida Na. 9330 ya 2025 | 18 Julai, 2025 | Kusogeza karibu huduma kwa wananchi na kuharakisha usikilizaji wa mashauri ya uhujumu uchumi. |

| Na. | JINA LA KANUNI | Na. ya Tangazo la Serikali | TAREHE YA KUINGIA KWENYE MATUMIZI | MANUFAA YAKE KWA UMMA |
|---|---|---|---|---|
| 4. | Kanuni za Ulinzi wa Mashahidi, 2025 | TS Na. 430 Mwaka 2025 | 11 Julai, 2025 | Kumlinda Shahidi dhidi ya vitisho au madhara mengine yoyote anayoweza kupata kwa sababu ya kutoa ushahidi Mahakamani.<br><br>Kuwezesha haki kutendeka kwa kuhakikisha mashuhuda wanatoa ushahidi pasipo kudhurika. |
| 5. | Kanuni za Mashauri ya Uchaguzi wa Wabunge, 2025 | TS Na. 431 Mwaka 2025<br><br>TS Na. 610 mwaka 2025 | 11 Julai, 2025<br><br>17 Oktoba, 2025 | Kutoa utaratibu wa usikilizwaji wa mashauri ya uchaguzi wa Wabunge haraka ipasavyo na kupunguza gharama na muda wa usikilizwaji wa mashauri hayo. |
| 6. | Kanuni za Mashauri ya Uchaguzi wa Madiwani, 2025 | TS Na. 433 Mwaka 2025<br><br>TS Na 611 Mwaka 2025 | 11 Julai, 2025<br><br>17 Oktoba, 2025 | Kutoa utaratibu wa usikilizwaji wa mashauri ya uchaguzi wa Madiwani haraka ipasavyo na kupunguza gharama na muda wa usikilizwaji wa mashauri hayo. |

| Na. | JINA LA KANUNI | Na. ya Tangazo la Serikali | TAREHE YA KUINGIA KWENYE MATUMIZI | MANUFAA YAKE KWA UMMA |
|---|---|---|---|---|
| 7. | The Judicature and Application of Laws (Constitutional Petitions) (Practice and Procedure) Rules, 2025 | GN No. 540 of 2025 | 5 Septemba, 2025 | Kuimarisha uwazi na kuongeza ubora wa maamuzi katika mashauri ya kikatiba yanayofunguliwa chini ya Ibara ya 108(2) ya Katiba.<br><br>Kuyapa uzito mashauri haya ya kikatiba kwa kuweka jopo la majaji watakaosikiliza wasipungue watatu |
| 8. | The Judicature and Application of Laws (Panel Constitution) Rules, 2025 | GN No. 541 of 2025 | 5 Septemba, 2025 | Kuimarisha ubora wa maamuzi kwenye mashauri yanayobeba masuala magumu ya kisheria na ushahidi (*complex legal and factual issues*) kwa kufanya mashauri hayo yasikilizwe na kuamuriwa na jopo la majaji wasiopungua watatu. |

| Na. | JINA LA KANUNI | Na. ya Tangazo la Serikali | TAREHE YA KUINGIA KWENYE MATUMIZI | MANUFAA YAKE KWA UMMA |
|---|---|---|---|---|
| 9. | The Civil Procedure Code (Amendment of the First Schedule), Rules 2025 | GN No. 569 of 2025 | 12 Septemba, 2025 | Kuongeza kasi ya usikilizaji wa maombi ya kutekeleza hukumu katika Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya kwa kuongeza wigo wa mahakimu wenye mamlaka ya kusikiliza maombi hayo.<br><br>Kupunguza mlundikano wa mashauri ya utekelezaji kwa Mahakimu Wafawidhi na hivyo kuongeza ufanisi.<br><br>Kuondoa ufisadi na matumizi mabaya ya mamlaka wakati wa utekelezaji wa tuzo (decree).<br><br>Kuleta uwajibikaji kwa maafisa watakaosikiliza maombi ya utekelezaji wa tuzo (decree).<br><br>Kuhakikisha michango ya Wafanyakazi inakusanywa na kufikishwa kwa wakati na Waajiri kwenye mifuko ya hifadhi za jamii kama ilivyokusudiwa.<br><br>Kuharakisha usikilizaji wa mashauri ya madai ya malimbikizo ya michango ya wafanyakazi kwa kupitia *summary procedure.* |

MAHAKAMA YA TANZANIA
JUDICIARY OF TANZANIA

| Na. | JINA LA KANUNI | Na. ya Tangazo la Serikali | TAREHE YA KUINGIA KWENYE MATUMIZI | MANUFAA YAKE KWA UMMA |
|---|---|---|---|---|
| 10. | The Judicature and Application of Laws (Defence Entitlement to Prosecution Evidence) Rules 2025 | GN No. 597 of 2025 | 3 Oktoba, 2025 | Kuimarisha haki ya usawa mbele ya sheria na haki ya kusikilizwa kwa ukamilifu kwa mujibu wa Ibara 13(1)(6)(a) ya Katiba.<br><br>Kuleta uwazi katika uendeshaji wa mashauri ya jinai yaliyoko Mahakama za Wilaya na Mkoa.<br><br>Kuzuia ubambikizaji wa kesi na kudhibiti vitendo vya rushwa.<br><br>Kuongeza ubora na uwajibikaji katika upelelezi wa makosa ya jinai.<br><br>Kuleta usawa mbele ya sheria baina ya upande wa mashtaka na mtuhumiwa na kupunguza Ushahidi wa kushtukiza *(ambush litigation)*. |

| Na. | JINA LA KANUNI | Na. ya Tangazo la Serikali | TAREHE YA KUINGIA KWENYE MATUMIZI | MANUFAA YAKE KWA UMMA |
|---|---|---|---|---|
| 11. | The Judicature and Application of Laws (Electronic Filing) (Amendment) Rules, 2025 | GN No. 609 of 2025 | 17 Oktoba, 2025 | Imehakikisha uthabiti wa sheria na kufanya sheria itabirike kwa sababu ukinzani ulioletwa na maamuzi ya Mahakama ya Rufani umetatuliwa na kwa sasa Wadaawa wanafahamu wazi wakati gani shauri linahesabika kufunguliwa. |

MAHAKAMA YA TANZANIA
JUDICIARY OF TANZANIA

**JEDWALI “G”: MAJENGO YANAYOKARABATIWA KWA AJILI YA KUANZISHA VITUO JUMUISHI VYA UTOAJI HAKI KWA MASHAURI YA MIRATHI, NDOA NA TALAKA**

| Na. | Jina la Jengo | Mahali lilipo | Hali ya sasa |
|---|---|---|---|
| 1. | Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma | Dodoma | Liko katika hatua za mwisho za ukarabati |
| 2. | Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza | Mwanza | Liko kwenye ukarabati |

MAHAKAMA YA TANZANIA
JUDICIARY OF TANZANIA

## JEDWALI “H”: TAKWIMU ZA MASHAURI YANAYOCHOCHEA UKUAJI WA UCHUMI YALIYOMALIZIKA 2025

| S/N | MAHAKAMA | IDADI NA AINA YA MASHAURI YALIYOMALIZIKA | | | | | | | THAMANI Tshs |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ARDHI | BENKI | KODI | BIASHARA | PSSF | NSSF | JUMLA | |
| 1. | Mahakama ya Rufani | 00 | 254 | 157 | 213 | 00 | 00 | 624 | 3,708,190,811,645 |
| 2. | Mahakama Kuu | 5,867 | 678 | 00 | 491 | 27 | 353 | 7,416 | 46,552,145,741,011 |
| 3. | Mahakama ya Hakimu Mkazi | 00 | 240 | 00 | 25 | 04 | 266 | 535 | 61,506,627,242 |
| 4. | Mahakama ya Wilaya | 00 | 278 | 00 | 47 | 02 | 100 | 427 | 119,865,095,064 |
| | Jumla ya mashauri | 5,867 | 1,450 | 157 | 776 | 33 | 719 | 9,002 | |
| | Thamani Tshs | 382,963,555,071 | 6,609,042,600,410 | 789,622,638,806 | 41,846,317,438, 318 | 7,688,245,498 | 813,762, 042,357 | | 50,441,708,274,962 |

MAHAKAMA YA TANZANIA

UHURU NA UMOJA

JUDICIARY OF TANZANIA